CHUO KIKUU CHA SOKOINE
CHA KILIMO

# MATUKIO YA SUA

*Januari - Machi, 2026*




**Toleo la 21**

**Ardhi ni Hazina**

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| 1 | Bodi ya Uhariri. |
| 2 | Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba aweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la taaluma na bweni SUA |
| 3 | SUA ina wigo mpana wa fursa za ajira na uwekezaji, Dkt. Bashiru |
| 4 | Maendeleo ya Teknolojia za Kidigitali kufungua fursa mpya za ajira kwa vijana nchini |
| 5 | Wanafunzi wa SUA Wapata Ujuzi wa Moja kwa Moja Katika Kubaini Magonjwa ya Mazao |
| 6 | Mfumo wa Afya ya Mnyama waendelea kuwasaidia wakulima |
| 7 | Wanafunzi SUA waendelea na utekelezaji wa mtaala unaolenga kuunganisha nadharia na vitendo |
| 8 | SUA Yazindua Mradi wa Kubadilisha Taka Hai kuwa Chakula cha Mifugo na Mbolea Hai |
| 9 | SUA Yakabidhi Rasmi Uendeshaji wa Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni |
| 10 | SUA yafufu soko la maua Mgeta, kituo cha wakulima chatazamwa kuwa kitovu cha wanunuzi |
| 11 | • Wanafunzi wanufaika wa MO-Kerry Scholarship waendelea na mafunzo<br>• SUA yaendelea kuwa karibu na wanafunzi wake kupitia huduma za ushauri wa kimasomo |
| 12 | SUA yakutana na wadau kujadili namna ya kuinua zao la karafuu |
| 13 | Kitengo cha Utafiti na Mafunzo ya Uchumi wa Buluu SUA |
| 14 | • SUA yaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia kwa maendeleo endelevu<br>• Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya yaupokea mwaka 2026 kwa kishindo |
| 15 | Tanzania kujifunza na kuimarisha matumizi bora ya mashine mbalimbali za kilimo |
| 16 | Ushirikiano wa Vyuo na Viawanda wapigiwa chapuo SUA |
| 17 | Inspekta Judith awataka wanafunzi kuvunja ukimya dhidi ya ukatili |
| 18 | • Fursa Mpya kwa Wanafunzi wa SUA<br>• Familia ya Dkt. Steven Mwakalinga yatembelea SUA |
| 19 | Mhe. Massawe aipongeza SUA kwa kuendelea kupanua maeneo ya Chuo<br>Dkt. Zacharia aongoza shughuli za upandaji miti SUA Kampasi ya Mizengo Pinda |
| 20 | • Prof. Mabiki awahimiza wanawake wa SUA kupima afya mapema<br>• Magonjwa yasiyoambukiza yaongezeka, Dkt. Chotamawe |
| 22 | Wanawake wa SUA waonesha upendo kwa jamii ya Kauzeni kupitia matendo ya huruma |
| 23 | SUA yaadhimisha Siku ya Wanawake kwa kuhimiza matumizi ya fursa za mafunzo |
| 24 | Warsha ya Uthibitishaji wa Mtaala wa PhD – REFOREST Africa |

# BODI YA UHARIRI

## WATAALAMU WA MAWASILIANO NA MASOKO

Bi. Suzana Magobeko
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**

Bw. Asifiwe Mbembela
**Afisa Mawasiliano na Masoko**

## MHARIRI

Prof. James Nyangas
**Mkuu wa Idara ya Elimu ya Saikolojia na Unasihi.**

## WASANIFU

Bw. Rajab Kimaro
Bi. Jackline Japhet

# Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba aweka jiwe la msingi la ujenzi wa jengo la taaluma na bweni SUA



Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kinaendelea kuimarisha miundombinu ya elimu katika Kampasi ya Mizengo Pinda kupitia ujenzi wa jengo la taaluma na bweni la wanafunzi kwa ufadhili wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), hatua inayolenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Akizungumza katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi, Mgeni Rasmi, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), alisema Serikali itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya elimu ya juu ili kuongeza ubora wa mafunzo, tafiti na huduma kwa jamii.

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma Prof. Maulid Mwatawala alieleza kuwa ujenzi wa jengo la taaluma na bweni katika Kampasi ya Mizengo Pinda utasaidia kuongeza uwezo wa chuo kupokea wanafunzi wengi zaidi pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunzia.



## HABARI PICHA

*Baadhi ya picha wakati wa ziara ya Waziri Mkuu Mhe. Mwigulu Nchemba katika Kampasi ya Mizengo Pinda*











# SUA ina wigo mpana wa fursa za ajira na uwekezaji, Dkt. Bashiru

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, ametoa rai kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi ya Wanyama, Viumbe Maji na Nyanda za Malisho kwamba hawatapoteza muda kwa kusoma katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwani sekta hizo zina wigo mpana wa fursa za ajira na uwekezaji.



Balozi Dkt. Bashiru aliyasema hayo alipokutana na wanafunzi wa mwaka wa pili wa Shahada ya Usimamizi wa Nyanda za Malisho waliokuwa kwenye mafunzo ya vitendo ya upandaji wa mbegu za malisho aina ya alfalfa, zenye uwezo wa kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa mifugo, wakati wa ziara yake ya siku moja chuoni hapo.

Katika mazungumzo hayo, aliwahimiza wanafunzi hao kuwekeza ipasavyo katika maarifa wanayoyapata kwa kuyafuatilia kwa umakini, ili waweze kung'amua na kutumia fursa zilizopo katika sekta ya nyanda za malisho, ambayo inaendelea kukua kutokana na ongezeko la mahitaji pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi.



Aidha, Balozi Dkt. Bashiru alisema Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimekuwa kikiiunga mkono Serikali katika utekelezaji wa sera na mikakati ya maendeleo, ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 inayosisitiza mabadiliko ya mifumo ya ufugaji kutoka wa kiasili kwenda ufugaji wa wanyama wachache wenye tija kubwa.

# Maendeleo ya teknolojia za kidigitali kufungua fursa mpya za ajira kwa vijana nchini

Washiriki wa kikao kazi cha utekelezaji wa Mradi wa Utafiti wa Majaribio kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) pamoja na VETA Dodoma, wamekutana kujadili mikakati ya kukuza ujuzi wa kidigitali kwa vijana ili kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa.

Mradi huo unalenga kuwajengea vijana uwezo wa kutumia elimu kuhusu teknolojia za kidigitali kama nyenzo ya kujikwamua kiuchumi, sambamba na kuonesha fursa zinazotokana na maendeleo ya teknolojia ya kidigitali.

Akizungumzia Mradi huo, Kiongozi wa mradi, Dkt. Alcardo Barakabitze kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia alisema Mradi unaenda kuwawezesha vijana elimu ya fursa za teknolojia kwa kipindi cha miezi mitatu, kisha kutathmini ufanisi wa elimu itakayotolewa kulingana na vijana watakavyofanya kazi baada ya uwezeshaji huo.

Akifungua kikao kazi hicho, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo - Taaluma, Prof. Maulid Mwatawala, alisema taasisi zinazoshiriki katika mradi huo zinapaswa kuhakikisha kuwa vijana wanaoishi katika jamii zinazozunguka vyuo hivyo wanakuwa wa kwanza kunufaika na mafunzo hayo, ili wawe kielelezo kwa wengine.

Aliongeza kuwa maendeleo ya kidigitali yameleta fursa nyingi za kiuchumi, ambapo vijana wanaweza kujiajiri kupitia ubunifu wa mawazo na miradi mbalimbali, hali itakayowawezesha kupata ufadhili kutoka kwa wadau tofauti.

Mradi wa utekelezaji wa utafiti wa majaribio katika teknolojia ya kidigitali kwa vijana unafadhiliwa na Benki ya Dunia ukilenga kuwaonesha vijana wa kitanzania fursa zinazopatikana kwa matumizi ya teknolojia mbalimbali za kidigitali.











# Wanafunzi wa SUA wapata ujuzi wa moja kwa moja matika kubaini magonjwa ya mazao





Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wakiwa wanashiriki mafunzo kwa vitendo ili kubaini magonjwa kwenye mazao yaliyopo kwenye mashamba ya mfano yanayopatikana katika Shamba la Mfano la SUA.

Mazoezi haya ya vitendo yanawawezesha wanafunzi kupata ujuzi wa moja kwa moja na kuelewa changamoto zinazowakabili wakulima, sambamba na mbinu bora za kushughulikia magonjwa ya mazao.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ni kitovu cha elimu ya kilimo nchini, kinachochangia katika maendeleo ya sekta ya kilimo na uchumi wa taifa.

Kupitia mafunzo, utafiti, na ushauri wa kitaalamu, Chuo kinasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao, kuimarisha usalama wa chakula, na kukuza teknolojia endelevu zinazoongeza tija ya wakulima. Hii inathibitisha nafasi muhimu ya Chuo katika kuendeleza uchumi wa viwandani na kilimo nchini Tanzania.



# Mfumo wa Afya ya Mnyama waendelea kuwasaidia wakulima

Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya, Prof. Esron Karimuribo, amewapongeza wabunifu wa Mfumo wa Afya ya Mnyama kwa kuendelea kuleta tija kwa wafugaji mbalimbali nchini, hususani katika kuwasaidia kutambua magonjwa na changamoto za mifugo yao hata wakiwa mbali na maeneo ilipo mifugo hiyo.

Mfumo huo ulioanzishwa mwaka 2024 na wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo umeendelea kuwa mkombozi kwa wafugaji ambapo kufikia mwishoni mwa mwaka 2025, mfumo huo ulikuwa umewahudumia zaidi ya wafugaji 1,000 katika mikoa ya Morogoro, Kagera na Shinyanga.

Kupitia mfumo huo, mifugo hufungwa tagi za kidijitali zinazotoa taarifa muhimu kwa msimamizi kuhusu hali ya afya ya mnyama, ikilinganishwa na njia ya asili ya kumuangalia kwa macho, ambayo mara nyingi husababisha baadhi ya magonjwa kubainika katika hatua za mwisho baada ya kuenea katika sehemu kubwa ya mwili.

Prof. Karimuribo alitoa pongezi hizo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake tarehe 29 Januari, 2026.





# Wanafunzi SUA waendelea na utekelezaji wa mtaala unaolenga kuunganisha nadharia na vitendo

Wanafunzi wa mwaka wa pili wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wanaosoma Shahada ya Familia na Sayansi ya Mlaji wanaendelea na mafunzo ya vitendo ya ushonaji, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mtaala unaolenga kuunganisha nadharia na vitendo katika mazingira halisi ya kazi.

Mafunzo hayo yanawawezesha wanafunzi kushiriki katika hatua mbalimbali za ushonaji, kuanzia upangaji wa malighafi, upimaji, ukataji hadi utengenezaji wa mavazi, hatua inayowajengea ujuzi wa kitaalamu, ubunifu na nidhamu ya kazi kulingana na viwango vya sekta husika.

Hatua hiyo inaonesha dhamira ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika kutoa elimu jumuishi inayomlenga mwanafunzi, kwa kuwajengea wahitimu ujuzi wa kujiajiri na kuajirika, sambamba na kuchangia maendeleo ya jamii na uchumi kupitia rasilimali watu yenye maarifa na uwezo wa vitendo.








# SUA yazindua mradi wa kubadilisha taka hai kuwa chakula cha mifugo na mbolea hai

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimezindua mradi wa kubadilisha taka hai kuwa chakula cha mifugo na mbolea hai, mradi unaolenga kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kukuza matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira.



Uzinduzi wa mradi huo ulifanyika Jumatano, Januari 28, 2026, katika Ukumbi wa ICE, ukihusisha wajumbe mbalimbali kutoka taasisi za elimu, watafiti na wadau wa mazingira.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mtafiti Mkuu wa mradi huo, Prof. Robert Max wa SUA, alisema mradi unatumia teknolojia ya mdudu aina ya Black Soldier Fly (BSF) kubadilisha taka hai kuwa rasilimali muhimu, ikiwemo chakula cha mifugo chenye ubora na mbolea hai.



Alieleza kuwa teknolojia hiyo husaidia kuboresha usimamizi wa taka na kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Prof. Max aliongeza kuwa utekelezaji wa mradi huo unaonesha dhamira ya SUA katika kuongoza tafiti bunifu zenye mwelekeo wa maendeleo endelevu, huku ukichangia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kukuza uchumi wa kijani na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

# SUA yakabidhi rasmi uendeshaji wa kituo cha taifa cha ufuatiliaji wa kaboni

Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kimekabidhi rasmi ofisi, vifaa pamoja na majukumu ya awali ya usimamizi wa kituo chataifa cha ufuatiliaji wa kaboni (NCMC) kwa Afisa Mtendaji Mkuu aliyeteuliwa wa Kituo hicho, hatua inayohitimisha rasmi jukumu la chuo katika awamu ya uanzishwaji wa taasisi hiyo ya kimkakati ya kitaifa.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Dkt. Richard Muyungi, alisema tukio hilo linaashiria dhamira ya Serikali ya kuhakikisha mpito wa kiutawala unafanyika kwa utaratibu, unaolinda mwendelezo wa majukumu na kuimarisha uwajibikaji katika usimamizi wa taasisi za umma.

Alieleza kuwa Serikali inatambua na kuthamini kwa kiwango kikubwa mchango wa SUA katika kuasisi na kusimamia Kituo hicho katika hatua zake za awali.

Dkt. Muyungi aliongeza kuwa Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni kilianzishwa rasmi kisheria Februari 2025, na katika kipindi cha mpito, SUA ilisimamia ujenzi na uimarishaji wa mifumo ya kiutawala, kitaasisi na kisheria, pamoja na kuratibu shughuli za mwanzo za ufuatiliaji wa kaboni nchini.

Hatua hizo zimeiweka NCMC katika nafasi nzuri ya kuanza utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi na kwa kuzingatia misingi ya uwazi na weledi.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda, alisema Chuo kitaendelea kushirikiana kwa karibu na Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni katika masuala ya kitaalamu, hususan kwenye biashara ya kaboni, utafiti na kujenga uwezo.

Alisisitiza kuwa ushirikiano huo ni muhimu katika kusaidia nchi kuibua, kusimamia na kutekeleza miradi ya kaboni itakayoongeza mapato ya taifa, kuchangia juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kunufaisha wananchi kupitia masoko ya kaboni.

Makabidhiano hayo yanafungua ukurasa mpya wa uendeshaji wa Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni, ambacho kinatarajiwa kuwa mhimili muhimu wa kitaifa katika kuratibu, kufuatilia na kusimamia masuala ya kaboni nchini kwa kuzingatia viwango vya kimataifa.












# SUA yafufua soko la maua Mgeta, kituo cha wakulima chatazamwa kuwa kitovu cha wanunuzi

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Ndaki ya Kilimo kimeanzisha mpango wa kufufua soko la maua fresh katika eneo la Mgeta kwa kulifanya Idara ya Ugani na Maendeleo ya Jamii Kituo cha Kilimo na Wakulima SUA Mgeta kuwa kitovu cha kuwaunganisha wakulima wa maua na wanunuzi wa maua kutoka ndani na nje ya nchi.

Kupitia ziara ya kitaalamu iliyofanyika kituoni hapo, SUA imewakutanisha wakulima wa Mgeta na wadau wa soko la maua ili kujadili mikakati ya kufufua zao hilo lenye fursa kubwa ya kiuchumi, kwa lengo la kupanua wigo wa vyanzo vya mapato kwa wakulima ambao kwa muda mrefu wamejikita zaidi katika kilimo cha mazao ya chakula.

Akizungumza katika mazungumzo hayo, Rasi wa Ndaki ya Kilimo SUA, Dkt. Nyambilila Amuri, alisema wanunuzi wa maua wapo tayari kununua mazao yatakayozalishwa na wakulima wa Mgeta, huku jukumu la SUA likiwa ni kuwawezesha wakulima hao kiufundi na kitaalamu ili wazalishe maua yanayokidhi viwango vya soko.

Kwa upande wake, Rais wa Shirikisho la Sanaa za Maonesho Tanzania, Dkt. Cynthia Henjewele, alisema changamoto ya upatikanaji wa maua imekuwa ikiwakabili wanunuzi, hali iliyowalazimu kutegemea maua kutoka Kenya na baadhi ya nchi za ukanda wa SADC, hivyo Mgeta ina fursa ya kipekee ya kuzalisha na kusambaza maua kwa soko la ndani na nje ya nchi.

Diwani wa Kata ya Nyandira ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, alisema elimu itakayotolewa na SUA kuhusu kilimo cha maua itaongeza uzalishaji wa kitaalamu, kuwasaidia wakulima kuwafikia wanunuzi moja kwa moja na kuchangia kukuza uchumi wa kaya kwa wananchi wa Mgeta.

Kwa upande wa wananchi Joseph Pastory kutoka Kata ya Nyandira na Philomena Oscar Mkule, walisema elimu hiyo iliyotolewa na wadau wa ununuzi wa maua kutoka Dar es Salaam kwa kushirikiana na wataalamu wa SUA imewaamsha na kuwahamasisha wakulima na vijana, wakiwemo wa kundi la Warriors Gang, kuchangamkia fursa ya kilimo cha maua kama njia ya kujikwamua kiuchumi.

# Wanafunzi wanufaika wa MO-Kerry Scholarship waendelea na mafunzo




Wanufaika 40 wa ufadhili wa Mo-Kerry Scholarship wanolewa mafunzo ya miezi minne ya nadharia na vitendo katika sayansi ya kilimo na chakula, yanayolenga kuwajengea washiriki maarifa ya kina, ujuzi na mbinu za kisasa katika eneo la chakula ili kuongeza ushindani na ufanisi wao katika soko la ajira na uzalishaji.

Mafunzo hayo yanafanyika katika Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro, chini ya usimamizi wa Dkt. Nuria Majaliwa, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ambaye anahakikisha maudhui ya mafunzo yanazingatia viwango vya kitaaluma na mahitaji halisi ya sekta husika.

Umuhimu wa mafunzo hayo ni mkubwa kwani yanawawezesha wanufaika kuunganisha nadharia na vitendo, kukuza ubunifu, na kuongeza uwezo wao wa kuchangia maendeleo ya sekta ya kilimo na usalama wa chakula nchini.

Kupitia mpango huo, washiriki wanapata maandalizi muhimu yatakayowawezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi katika mazingira ya viwanda na uzalishaji wa kisasa.






# SUA yaendelea kuwa karibu na wanafunzi wake kupitia huduma za ushauri wa kimasomo

Kaimu Mshauri wa Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Bi. Hilda Gamuya, alizungumza na wanafunzi waliofika ofisini kwake kuomba ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya masomo yao.

Zoezi hilo lilifanyika leo Januari 09, 2025, katika Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro, likiwa ni sehemu ya utaratibu wa kawaida wa chuo wa kuwapokea na kuwasikiliza wanafunzi.

Katika kikao hicho, Bi. Gamuya aliwasikiliza wanafunzi kwa makini na kutoa ushauri unaolenga kuwasaidia kutatua changamoto za kimasomo wanazokabiliana nazo, huku akiwahimiza kuendelea kuwa na nidhamu na ili kuboresha maendeleo yao ya kitaaluma.

Hatua hii inaendelea kuonesha dhamira ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika kuhakikisha ustawi wa wanafunzi wake, si tu kielimu bali pia kisaikolojia na kijamii. Chuo kinastahili pongezi kwa kuendelea kuweka mifumo rafiki ya ushauri na msaada, inayowasaidia wanafunzi kufikia ndoto na malengo yao ya kitaaluma na maisha kwa ujumla.





# SUA yakutana na wadau kujadili namna ya kuinua zao la karafuu

Katika kuadhimisha miaka 200 ya zao la karafuu duniani, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimekutana na wadau mbalimbali wanaojihusisha na uendelezaji wa zao la karafuu, kwa lengo la kujadili njia na mikakati ya kuinua na kuhamasisha jamii kutambua fursa zinazopatikana katika zao hilo, linalotajwa kuwa miongoni mwa mazao ya kimkakati katika Mkoa wa Morogoro.

Akizungumza baada ya kikao hicho, Rasi wa Ndaki ya Kilimo, Dkt. Nyambilila Amuri, alisema kikao hicho kimejikita katika kujadili namna ya kulienzi na kulifufua zao la karafuu ili liwe chachu ya maendeleo na chanzo cha kipato kwa wakulima pamoja na wananchi wa Mkoa wa Morogoro kwa ujumla.

Dkt. Nyambilila alisema Ndaki ya Kilimo imeona fursa kubwa katika zao hilo, kwani limo katika ajenda ya ufundishaji kama mojawapo ya mazao ya viungo (spice crops) yanayofundishwa chuoni hapo.

Aliongeza kuwa karafuu ni zao lenye thamani kubwa kiuchumi, hivyo kukutana na wadau hao ni hatua muhimu katika kuimarisha ushirikiano na kuendeleza tafiti pamoja na mipango ya maendeleo ya zao hilo.

Kwa upande wake, Mwanzilishi na Mfawidhi wa Shirika la Umoja Conservation Trust, Bw. Bryan Bwana, alisema wamefika SUA kwa lengo la kuanzisha ushirikiano wa pamoja, ikiwemo kubuni sera na mikakati kabambe ya kukuza zao la karafuu. Amesema zao hilo lina faida nyingi kwa wananchi, na anaamini ushirikiano huo utafanikiwa kwa kuwa SUA ni chuo kikongwe chenye wataalam wabobezi katika nyanja mbalimbali za sekta ya kilimo.

Kikao hicho kiliwakutanisha wadau mbalimbali akiwemo Umoja Conservation Trust, Tanzania Environmental Expert Association pamoja na wanataaluma kutoka SUA.

Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni kuanzishwa kwa matukio ya kijamii na michezo kama Karafuu Cup na Karafuu Marathon, pamoja na kuendeleza utalii wa karafuu, kwa lengo la kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu fursa zilizopo katika zao hilo linalolimwa kwa wingi Zanzibar na pia Tanzania Bara hususani Mkoa wa Morogoro.



# Kitengo cha Utafiti na Mafunzo ya Uchumi wa Buluu SUA

Kitengo cha Utafiti na Mafunzo ya Uchumi wa Buluu cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ni kitengo cha kitaaluma kinacholenga kuendeleza maarifa, ujuzi na tafiti bunifu katika sekta ya uchumi wa buluu, hususan katika uzalishaji, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za majini.

Kitengo hiki kina jukumu muhimu katika kuandaa wataalamu wenye uwezo wa kukabiliana na changamoto na fursa zilizopo katika sekta ya viumbe wa majini kwa kuzingatia misingi ya sayansi, teknolojia na maendeleo endelevu.

Kupitia mtaala unaojumuisha nadharia na mafunzo ya vitendo, kitengo hiki huwajengea wanafunzi na watafiti uelewa mpana wa masuala ya uzalishaji wa samaki, ufugaji wa viumbe wa majini, usimamizi wa mifumo ikolojia ya majini, pamoja na masuala ya uchumi, sera na masoko yanayohusiana na uchumi wa buluu.

Mafunzo yanatolewa kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa, sambamba na mahitaji ya sasa ya sekta husika. Kwa upande wa vitendo, kitengo hutoa mafunzo ya kina yanayohusisha hatua zote muhimu za uzalishaji wa viumbe wa majini, ikiwemo uandaaji wa mabwawa na miundombinu ya uzalishaji, uzalishaji na ufugaji wa vifaranga, ulishaji sahihi, udhibiti wa magonjwa, pamoja na ufuatiliaji wa ukuaji, ubora na tija ya mazao ya majini.

Aidha, wanafunzi hushiriki katika tafiti shirikishi zinazolenga kuboresha teknolojia za uzalishaji na kuimarisha matumizi endelevu ya rasilimali za majini.

Kwa ujumla, Kitengo cha Utafiti na Mafunzo ya Uchumi wa Buluu cha SUA kinaendelea kuwa kitovu cha umahiri wa kitaaluma na kisayansi, kikichangia katika maendeleo ya rasilimali watu, uzalishaji wa maarifa na utoaji wa suluhisho endelevu kwa ajili ya kukuza uchumi wa buluu nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki.









# SUA yaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia kwa maendeleo endelevu




Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeendelea kudhihirisha dhamira yake ya dhati katika kuandaa rasilimali watu mahiri kupitia mifumo bora ya ufundishaji na ujifunzaji inayozingatia mahitaji ya sasa na ya baadaye ya maendeleo ya taifa.

Moja ya maboresho ni katika mitaala yenye mwelekeo wa vitendo, tafiti na ubunifu, SUA kimekuwa Chuo chenye kutoa elimu inayowawezesha wanafunzi kupata maarifa, stadi na ujuzi unaokidhi matakwa ya soko la ajira na kujiajiri, hususan katika sekta za kilimo, sayansi, teknolojia na maendeleo ya jamii.

Uimarishaji huo, SUA kimewekeza kwa kiwango kikubwa katika miundombinu ya kisasa ya kufundishia na kujifunzia, ikiwemo mashamba darasa, pamoja na maabara zilizoimarishwa kwa vifaa na vitendea kazi vya kisasa.

Aidha, mafanikio hayo yamewezeshwa kwa kiasi kikubwa na jitihada za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo imeendelea kuwekeza katika elimu ya juu kwa kuboresha miundombinu, rasilimali watu na mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia.



# Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya yaupokea mwaka 2026 kwa kishindo



Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) imeukaribisha mwaka 2026 kwa kishindo kupitia hafla maalum iliyolenga kukumbushana majukumu ya kazi, kupongezana kwa utendaji wa mwaka uliopita, pamoja na kuwaaga watumishi waliomaliza muda wao katika utumishi wa umma.

Hafla hiyo ilifanyika tarehe 22 Januari, 2026 katika viwanja vya Ndaki hiyo ambapo mgeni rasmi alikuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Prof. Maulid Mwatawala. Tukio hilo liliwakutanisha viongozi, wahadhiri na watumishi wa Ndaki katika mazingira ya mshikamano na tafakari ya pamoja kuhusu mwelekeo wa kazi kwa mwaka mpya.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Mwatawala aliipongeza Ndaki hiyo kwa kuendeleza utamaduni wa kuandaa hafla za aina hiyo, akisisitiza kuwa ni nyenzo muhimu katika kuimarisha ustawi wa wafanyakazi, kujenga mshikamano kazini, na kuongeza ari ya uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kitaaluma na kiutawala.

Kwa upande wake, Rasi wa Ndaki, Prof. Esron Karimuribo, alisema kuwa hafla hiyo hufanyika kila mwaka kama jukwaa la kutathmini, kujifunza na kupongezana katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ndaki, ikiwemo ufundishaji, utafiti na huduma kwa jamii. Aliongeza kuwa mwanzo wa mwaka ni fursa muhimu ya kutoa dira, malengo na mwelekeo wa pamoja kwa mwaka mzima wa kazi.

Aidha, Prof. Karimuribo alibainisha kuwa mwaka 2026 ni wa kihistoria kwa Ndaki ya VET, kwani inaelekea kutimiza miaka 50 tangu kuanzishwa kwake. Alieleza kuwa katika kipindi hicho Ndaki imepata mafanikio makubwa pamoja na kukabiliana na changamoto mbalimbali, ambazo ni somo muhimu katika kupanga mikakati na kuboresha utekelezaji wa majukumu yake.

# Tanzania kujifunza na kuimarisha matumizi bora ya mashine za kilimo

Ili kuifanya sekta ya kilimo kuwa na mchango mkubwa zaidi katika pato la mwananchi mmoja mmoja na uchumi wa taifa kwa ujumla, Tanzania inalenga kujifunza na kuimarisha matumizi bora ya mashine mbalimbali za kilimo, pamoja na kuzishirikisha taasisi za kielimu kama SUA ili zisaidie katika kufanya tafiti pamoja na kutoa wahitimu bora.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Peter Msofe, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Uendelezaji wa Mazao na Usalama wa Chakula, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa jukwaa la kubadilishana uzoefu kati ya Tanzania na Japan.

Jukwaa hilo liliandaliwa kupitia Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), ambapo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo inashiriki kupitia wanataaluma na wanafunzi wake.

Alisema kuwa Tanzania inapitia mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo, hususan baada ya kupitishwa kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

Kupitia dira hiyo, Tanzania inalenga kuharakisha ukuaji wa uchumi ili pato la taifa lifikie dola trilioni moja ifikapo mwaka 2050, huku pato la mwananchi wa kawaida likifikia dola za Kimarekani 7,000, na taifa kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati cha juu.

Prof. Msofe alisisitiza kuwa malengo hayo hayawezi kufikiwa bila kuipa kipaumbele sekta ya kilimo.

Alieleza kuwa ili kilimo kiwe na tija, ni lazima kibadilike kutoka kilimo cha asili na kuelekea kilimo cha kisasa kinachotumia mashine.

Katika kufanikisha hilo, Serikali imeamua kuanzisha zaidi ya vituo 1,000 nchi nzima ambavyo vitahifadhi mashine za kilimo, kutoa huduma za matengenezo, na kuwezesha wakulima kupata mashine hizo kwa urahisi.

Aidha, vituo hivyo vitasaidia katika usambazaji wa pembejeo, ikiwemo mbolea, pamoja na utekelezaji wa mipango ya ruzuku ya kilimo, hatua inayolenga kuongeza uzalishaji, kuboresha kipato cha wakulima, na kuchochea maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo nchini.












*Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Philemon Wambura (kushoto) akizungumza na Mwandishi Mwandamizi wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko na Kituo cha Redio cha SUA FM (101.1), Bi. Farida Mkongwe.*

# Ushirikiano wa Vyuo na Viwanda wapigiwa chapuo SUA

Wakati siku chache zikiwa zimepita tangu Serikali izindue Mpango wa Ushirikiano kati ya Vyuo na Viwanda, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Philemon Wambura, amesema endapo kila taasisi, ikiwemo SUA, italibeba jambo hilo kwa mtazamo chanya, litachochea mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu nchini.

Prof. Wambura aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na SUAMEDIA katika mahojiano maalum kuelekea maadhimisho ya miaka 50 ya Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya, yanayotarajiwa kuadhimishwa Novemba 2026, ambapo alisema licha ya kuwapo kwa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika elimu ya vyuo nchini, urasimishaji wa mpango huo unahitaji msukumo zaidi ili kuimarisha ushirikiano wa karibu na wenye tija.

Alifafanua kuwa ni muhimu kwa viwanda kueleza kwa uwazi mahitaji yao kwa wahitimu, ili vyuo viandae mitaala inayozingatia mabadiliko ya soko la ajira, akisisitiza umuhimu wa elimu inayojikita katika vitendo kwa wanafunzi, ili kuwawezesha kuwahudumia ipasavyo wafugaji, wakulima na wavuvi nchini.

Kwa upande wake, SUA imeendelea kuboresha mitaala yake kwa kuruhusu viwanda kushiriki moja kwa moja katika ufundishaji, hatua inayowapa wanafunzi fursa ya kujifunza mahitaji mahsusi ya kada zao kutoka kwa wadau wa sekta ya uzalishaji.

Kupitia mpango huo, maboresho yameonekana katika maeneo mbalimbali ikiwemo maendeleo ya Idara ya Shamba la Mafunzo, Idara ya Sayansi ya Viumbe Maji, Utafiti na Nyanda za Malisho pamoja na Kitengo cha Ushonaji wa mitindo mbalimbali, ambavyo vinawawezesha wanafunzi kushiriki kikamilifu kwa vitendo katika shughuli za mafunzo.





# Inspekta Judith awataka wanafunzi kuvunja ukimya dhidi ya ukatili

Inspekta Judith Mbukwa, Mratibu wa Mkoa wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi Katavi, amewahimiza wanafunzi kutumia mifumo rasmi ya kuripoti matukio ya ukatili na unyanyasaji badala ya kukaa kimya au kubaki na maumivu moyoni.

Alitoa wito huo alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa Ndaki ya Kampasi ya Mizengo Pinda, akisisitiza kuwa kila mwanafunzi ana haki ya kusoma katika mazingira salama na yenye heshima.

Akieleza umuhimu wa Dawati la Jinsia, Inspekta Mbukwa aliwahamasisha wanafunzi kulifikia pindi wanapokumbana na changamoto kama unyanyasaji wa kijinsia, vitisho, dhuluma au manyanyaso ya aina yoyote. Alisisitiza kuwa taarifa zinapotolewa mapema, husaidia mamlaka kuchukua hatua stahiki kwa haraka huku zikilinda usiri na usalama wa mhanga.

Aidha, alibainisha kuwa malalamiko mengi yanayopokelewa yanahusisha ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia pamoja na vitendo vya ubaguzi na vitisho. Aliwataka wanafunzi kuvunja ukimya, kuondoa hofu na kujenga utamaduni wa kusaidiana, akieleza kuwa ukimya humlinda mhalifu na huongeza madhara kwa mwathirika na jamii kwa ujumla.

Aliwahimiza wanafunzi kuwa mabalozi wa maadili kwa wenzao kwa kutoa msaada, ushauri na kuhamasishana kuripoti vitendo vya ukatili.

Alisisitiza kuwa ushirikiano kati ya wanafunzi, uongozi wa taasisi na vyombo vya dola ni msingi muhimu wa kujenga kampasi salama, yenye kuheshimu haki za binadamu na kuimarisha mafanikio ya kitaaluma.



# Fursa mpya kwa wanafunzi wa SUA



Wanafunzi wa SUA wanatarajiwa kunufaika na mkataba mpya wa ushirikiano uliosainiwa kati ya SUA, KOKOA KAMILI na AGCOT, unaolenga kuendeleza mnyororo wa thamani wa kokoa kuanzia shambani hadi viwandani.

Kwa mujibu wa viongozi wa taasisi hizo, ushirikiano huo utatoa mafunzo ya vitendo, programu za mafunzo kazini, na miradi ya utafiti itakayolenga kutatua changamoto za uzalishaji na masoko ya kakao.

Mkurugenzi wa KOKOA KAMILI, Simran Bindra, alisema uzoefu wake wa zaidi ya muongo mmoja katika sekta ya kokoa unaonesha kuwa Tanzania ina moja ya kokoa bora duniani, na juhudi za pamoja zitasaidia kuiweka nchi katika nafasi ya ushindani mkubwa zaidi kimataifa.

Aidha, makubaliano hayo yanatarajiwa kuchochea uwekezaji katika sekta ya kokoa, kuongeza ajira kwa vijana na kuinua uchumi wa wakulima kupitia teknolojia bora na maarifa mapya.



# Familia ya Dkt. Steven Mwakalinga yatembelea SUA



Familia ya marehemu Dkt. Steven Mwakalinga imetembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa lengo la kuenzi historia ya elimu yake na kutambua mchango wake mkubwa alioutoa katika nyanja ya taaluma wakati wa uhai wake.

Katika ziara hiyo, familia ilieleza mchango na nafasi ya kipekee katika safari ya kielimu na kitaaluma ya marehemu Dkt. Mwakalinga, hivyo kuona ni vyema kurejea chuoni hapo kama sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu na kuendeleza urithi wake wa elimu.

“Kabla ya kufariki mume wangu alituahidi kuwa siku moja atatupeleka Tanzania kutuonesha Chuo kilichomfanya kuwa bora kwa miaka mitano (5), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo", alisimulia kwa majonzi aliyekuwa mke wake Bi. Edith Chenga Chamwi ambaye alisema ndoto hiyo imewasukuma kufunga safari na kufika hapa SUA ili kuona yale ambayo alikuwa anawaeleza kabla ya kifo chake.

Dkt. Mwakalinga alifariki Dunia Mei 02, 2025 katika Hospitali ya Bispebjer chini Copenhagen wakati akiendelea kupatiwa matibabu, ambapo safari yake ya kimasomo SUA, ilianza mwaka 1997 - 2002 ambapo alisomea Shahada ya Sayansi katika Tiba ya Wanyama.

Ziara hiyo ilionesha mshikamano uliokuwepo kati ya familia na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, huku ikitumika kama mfano wa kutambua mchango wa wahitimu waliolitumikia taifa kupitia elimu waliyoipata chuoni hapo.



# Mhe. Massawe aipongeza SUA kwa kuendelea kupanua maeneo ya Chuo

Kutokana na ongezeko la watu nchini Tanzania, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Mhe. Andrew Massawe, amepongeza juhudi za upanuzi wa maeneo ya Chuo hicho, akisema kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kukidhi ongezeko la mahitaji ya miundombinu ya elimu, tafiti na mafunzo kwa vitendo.

Mhe. Massawe alitoa pongezi hizo baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Prof. Agnes Sirima, Rasi wa Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii ambayo imeeleza kuwa mbali na Msitu wa Mafunzo wa Olmontonyi pia Chuo kinaendelea kutanua maeneo yake ya mafunzo katika mikoa mbalimbali likiwemo eneo la Ifinga, Ruvuma.

Prof. Sirima alisema eneo la Ifinga zoezi la kupanda miti linaendelea baada ya kukamilika litaongeza wigo wa wanafunzi kujifunza na kusaidia kuongeza mapato ya Chuo.

Kufuatia taarifa hiyo, Mhe. Massawe alisema ni hatua nzuri kwa Chuo kwani mahitaji ya sasa hayatakuwa sawa na labda mwaka 2050 ambapo watu watakuwa wameongezeka maradufu na mahitaji ya elimu yanaweza kuwa yamebadilika pia.

Ziara hiyo ni mwendelezo wa ziara anazoendelea kuzifanya Mhe. Massawe baada ya kuteuliwa kushika nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza la Chuo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.



# Dkt. Zacharia aongoza shughuli za upandaji miti SUA Kampasi ya Mizengo Pinda



Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Kampasi ya Mizengo Pinda, Dkt. Zacharia Malley, ameongoza shughuli ya upandaji miti katika kampasi hiyo kama ishara ya kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuhifadhi mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Zoezi hilo lilifanyika chini ya kauli mbiu ya kitaifa "Mti Wangu, Taifa Langu," kampeni iliyoanzishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, yenye lengo la kurejesha uasili wa mazingira, kuongeza uoto wa asili na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Dkt. Zacharia Malley alisisitiza kuwa upandaji miti ni uwekezaji wa muda mrefu kwa vizazi vijavyo, akibainisha kuwa vyuo vya elimu ya juu vina wajibu wa kuongoza kwa vitendo katika juhudi za uhifadhi wa mazingira, akisema SUA itaendelea kushiriki kikamilifu katika miradi inayolenga kulinda mazingira na kuhimiza jamii kuiga mfano huo.

Kwa upande wake, Rasi wa Ndaki katika Kampasi ya Mizengo Pinda, Prof. Anna Sikira, alisema kampasi hiyo imejipanga kuhakikisha miti yote inayopandwa inatunzwa na kusimamiwa ipasavyo hadi ikue, kwa lengo la kutengeneza mazingira rafiki kwa shughuli za kimasomo, utafiti na ustawi



# Prof. Mabiki awahimiza wanawake wa SUA kupima afya mapema



Wanawake wametakiwa kupima afya zao mara kwa mara ili kugundua mapema magonjwa hatari kama saratani ya shingo ya kizazi na saratani ya matiti, hatua itakayosaidia kuokoa maisha na kupunguza madhara yanayoweza kuzuilika.

Wito huo ulitolewa na Mkemia na Mtafiti wa Miti Dawa kutoka SUA, Prof. Faith Mabiki, alipokuwa akizungumza katika kongamano maalum la afya ya wanawake lililofanyika chuoni hapo.

Prof. Mabiki alisema wanawake wengi bado huweka afya zao kama jambo la pili kutokana na hofu au ukosefu wa taarifa sahihi, hali inayoweza kusababisha madhara makubwa yanayozuilika.

"Kuna hofu kubwa miongoni mwa wanawake kuhusu vipimo vya afya, lakini teknolojia ya kisasa imerahisisha uchunguzi na kutoa matokeo sahihi bila usumbufu mkubwa. Ni bora kugundua mapema, kutibiwa na kuendelea na maisha yenye afya njema," alisema Prof. Mabiki.

Alisisitiza kuwa mwanamke mwenye afya bora huongeza tija katika familia, kazini na katika jamii kwa ujumla, hivyo kuchangia maendeleo ya taifa.



# Magonjwa yasiyoambukiza yaongezeka, Dkt. Chotamawe



Daktari wa watoto katika Hospitali ya SUA, Dkt. Graca Chotamawe, amesema magonjwa yasiyoambukiza yanaendelea kuwa tishio kubwa duniani na barani Afrika.

Akitoa mada katika kongamano la afya ya wanawake lililofanyika SUA, Dkt. Chotamawe alisema takribani watu milioni 41 hupoteza maisha kila mwaka duniani kutokana na magonjwa yasiyoambukiza, huku barani Afrika magonjwa hayo yakiongezeka kwa kasi.

Alieleza kuwa sababu kuu za ongezeko hilo ni mabadiliko ya mtindo wa maisha, kupungua kwa kufanya mazoezi, kuongezeka kwa matumizi ya magari, bodaboda na bajaji, matumizi ya dawa za kulevya, mabadiliko ya mifumo ya kilimo pamoja na umasikini.

Aidha, aliongeza kuwa magonjwa yasiyoambukiza huongeza mzigo wa kiuchumi kwa familia nyingi kwa kuwa ni ya muda mrefu na huhitaji gharama kubwa za matibabu, jambo linaloweza kusababisha watu wengi kuangukia katika umasikini.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na watumishi wanawake wa SUA pamoja na wanafunzi, likiwa ni sehemu ya juhudi za kuongeza uelewa, kuhamasisha uchunguzi wa mapema na kujenga utamaduni wa kujali afya miongoni mwa wanawake.



# HABARI PICHA

*Wanafunzi wa SUA wakiwa katika Vimbweta, madarasa na Maktaba ya Taifa ya Sokoine ya Kilimo ikiwa ni maandalizi ya mtihani wa muhula wa kwanza wa mwaka wa masomo 2025/2026.*










# HABARI PICHA

*Watumishi wanawake wa SUA katika Ndaki ya Kampasi ya Mizengo Pinda mkoani Katavi walipoadhimisha Siku ya Wanawake Duniani 2026 kwa kuwatembelea akina mama waliopo katika wodi ya wazazi (waliojifungua) katika Kituo cha Afya Usevya. Katika ziara hiyo waliwapatia zawadi mbalimbali kama ishara ya upendo, mshikamano na kujali ustawi jamii.*







# Wanawake wa SUA waonesha upendo kwa jamii ya Kauzeni kupitia matendo ya huruma










Wanawake wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na wafanyakazi wengine wa chuo hicho wamefanya matendo ya huruma kwa kutoa misaada ya vitu mbalimbali ikiwemo nguo, sukari, unga, sabuni na mafuta kwa wahitaji wa Kata ya Kauzeni iliyopo Manispaa ya Morogoro pamoja na Kituo cha Watoto cha Sarafina kilichopo katika kata hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, kwa lengo la kuonesha upendo na mshikamano kwa jamii.

Akizungumza wakati alipokabidhi misaada hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake wa Chama cha Wafanyakazi RAAWU Tawi la SUA ambaye pia ni mratibu wa shughuli hiyo, Bi. Enessa Mlay, alisema wanawake wa SUA wameona umuhimu wa kuadhimisha siku hiyo kwa vitendo kwa kuwafikia wananchi wanaohitaji msaada ili kuonesha mshikamano kwa jamii kwa kufanya matendo ya huruma.

"Kipindi hiki ni cha mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani na Kwaresima, ambacho tunahimizwa kufanya matendo mema na kusaidiana katika jamii, lengo letu kubwa ni kuacha alama ya upendo na kuwakumbusha wananchi kuwa SUA ipo karibu nao na inaendelea kujali ustawi wa jamii inayowazunguka", alisema Bi. Mlay.

Kwa upande wake, Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Kauzeni, Vicent Zakaria Katabi, aliwashukuru wanawake na wafanyakazi wa SUA kwa moyo wao wa kujitoa kusaidia jamii na kwamba msaada huo umeleta faraja kubwa kwa wananchi wa Kauzeni na ni mfano mzuri wa kuigwa na wadau wengine, huku akisisitiza kuwa kufanya matendo ya huruma ni ibada na kunaleta faraja kwa wale wanaohitaji msaada.

Naye Mratibu wa tawi la Shirika la SAFINA Street Network Morogoro, Amani Evarist Kumba, aliwashukuru wanawake wa SUA kwa msaada wao na kuwataka wawe mabalozi wazuri wa kuitangaza taasisi hiyo inayofanya kazi ya kuwasaidia watoto na vijana waliowahi kuishi na kufanya kazi mitaani ili wadau zaidi waweze kujitokeza na kuwawezesha katika mahitaji mbalimbali.

Alisema kwa sasa shirika hilo ambalo lina matawi katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Singida na Dodoma, kwa mwaka huu linawahudumia watoto 40 mkoani Morogoro kwa kuwapatia huduma za chakula, mavazi, matibabu na elimu kuanzia shule ya msingi hadi chuo.

Kwa upande wake, mkazi wa Kata ya Kauzeni, Aziza Ally Kilongola, alitoa shukrani kwa wanawake wa SUA kwa msaada walioutoa akisema umeleta faraja kwa wanufaika na jamii kwa ujumla.

# SUA yaadhimisha Siku ya Wanawake kwa kuhimiza matumizi ya fursa za mafunzo

Wanawake wametakiwa kutumia kikamilifu fursa za masomo na mafunzo zinazotolewa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ili kujijengea uwezo, kuongeza ujuzi na kuimarisha ushiriki wao katika maendeleo ya jamii.

Wito huo ulitolewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Amandus Muhairwa, wakati wa hafla ya kuwapongeza wanawake wa chuo hicho katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kwenye ukumbi wa SUA uliopo Nanenane mjini Morogoro.

Prof. Muhairwa alisema kuwa SUA ina mfumo thabiti wa kulinda wanawake na wasichana pamoja na kutekeleza mpango mkakati wa usawa wa kijinsia, hali inayochangia kuwepo kwa mazingira salama na yenye utulivu yanayowezesha wanawake kufikia malengo yao ya kitaaluma na kiutendaji.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Makamu Mkuu wa Chuo ambaye pia ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Prof. Maulid Mwatawala, alisema kuwa katika uongozi wa Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda, wanawake wameendelea kupata nafasi zaidi za uongozi chuoni huku wanafunzi wa kike wakionesha kufanya vizuri kitaaluma.

Prof. Mwatawala alisema kwa sasa chuo kimefikia asilimia 43 katika kuelekea lengo la usawa wa kijinsia wa asilimia 50 kwa 50. Aidha, amewapongeza wanawake kwa juhudi zao katika kazi na mchango wao katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kwa upande wao, Mwenyekiti wa RAAWU tawi la SUA, Bw. Faraja Kamendu, na Mwenyekiti wa THTU tawi la SUA, Bw. Nickson Mkilamwene, walisema kuwa kuwapa wanawake nafasi katika ajira na uongozi kunachochea ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi mbalimbali.

Viongozi hao pia waliwahamasisha wanawake kufanya kazi kwa bidii kwa maendeleo ya chuo na kujiunga na vyama vya wafanyakazi ili kulinda maslahi yao ya kikazi na kitaaluma.









# Warsha ya Uthibitishaji wa Mtaala wa PhD – REFOREST Africa

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), kupitia Mradi wa REFOREST Africa, kimefanikiwa kuandaa Warsha ya siku mbili ya Uthibitishaji wa Mtaala wa Shahada ya Uzamivu (PhD) jijini Arusha. Warsha hiyo iliwakutanisha wataalamu wa kitaaluma, watafiti, na wadau wa sekta ya misitu kwa lengo la kupitia, kuboresha, na kuthibitisha mtaala ili kuhakikisha unakidhi viwango vya juu vya kitaaluma na mahitaji ya sasa na ya baadaye ya Afrika katika usimamizi endelevu wa misitu na mazingira.

Warsha ilijumuisha mijadala shirikishi, mawasilisho ya kitaalamu, na uchambuzi wa kina wa maudhui ya mtaala. Kupitia michango ya wadau, mtaala uliimarishwa ili uwe na mwelekeo wa vitendo, unaojibu changamoto halisi za sekta ya misitu na kuandaa wataalamu watakaotoa suluhu endelevu kwa masuala ya mazingira na maendeleo barani Afrika.

Hatua muhimu ya warsha ilikuwa Uthibitisho wa Wadau (Stakeholders Validation), ambapo wawakilishi kutoka vyuo vikuu, taasisi za serikali, na sekta ya misitu walithibitisha rasmi kuwa mtaala wa PhD wa REFOREST Africa ni husika, unaendana na vipaumbele vya kikanda na bara, na unakidhi mahitaji ya soko la ajira na jamii kwa ujumla.

Kwa mtazamo wa kimkakati, programu ya PhD ya REFOREST Africa inalenga kuimarisha uwezo wa Afrika katika kuzalisha watafiti na wataalamu wabobezi wa misitu wenye ujuzi wa hali ya juu, tafiti zenye athari, na uwezo wa kuongoza mabadiliko katika sera na vitendo vya usimamizi wa rasilimali za misitu, hususan katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uhifadhi wa bioanuwai.

Mradi wa REFOREST Africa, unaoongozwa na Prof. Romanus Ishengoma, unaweka mkazo katika usawa wa kijinsia kwa kuweka mazingira rafiki na mifumo ya msaada kwa wanawake wanaosomea Shahada ya Uzamivu. SUA inaishukuru kwa dhati Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uswidi (Sida) kwa ufadhili na ushirikiano wake endelevu unaochangia kuimarisha elimu na tafiti za misitu barani Afrika.










## HABARAI PICHA

***Baadhi ya Watumishi Waumini wa Dini ya Kiislamu wakiwa katika Ukumbi wa Multipurpose uliopo Kampasi ya Edward Moringe, Morogoro wakishiriki hafla ya Iftar iliyoandaliwa na Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda Machi 13, 2026, kama sehemu ya kuimarisha mshikamano na kudumisha utamaduni wa kushirikiana katika matukio muhimu ya kijamii na kiimani.***













# MATANGAZO

## KARIBU UTANGAZE NA SUA FM, 101.1

*Kwa Gharama Nafuu*




*@sokoineuniversityofagriculture*

*@SokoineU*

*Kwa Mawasiliano piga simu*

**0655424251**
**0655370047**

# UTALII

## KARIBU UTEMBELEE KAMPASI ZA SUA KWA UTALII NA KUJIFUNZA















**Jarida limeandaliwa na:**
**Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**
**S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania**
**Simu: 255-023-2640006/7/8/9,**
**Baruapepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz**